

HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA.

**SHULE YA SEKONDARI KIPETA,
S.L.P 78,
SUMBAWANGA.**

1.12.2020

Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi :

.....

S.L.P

.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIPETA HALMASHAURI YA SUMBAWANGA MKOA WA RUKWA MWAKA 2019.

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanaao amechaguliwa kijiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari kipeta mwaka 2021. Shule ya Sekondari Kipeta ipo umbali wa kilometri 176 Mashariki mwa mji wa Sumbawanga. Usafiri wa basi kutoka Sumbawanga mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Sumbawanga Nauli ni shilingi 20,000/= tu hadi kipeta sekondari. Njia nyingine ya kupita ni kuanzia mlowo-Vwawa iliyoko katika mkoa wa Songwe, nauli yake ni 10,000/= tu hadi yanapoishia mabasi (KILYAMATUNDU). Kutoka yanapoishia mabasi nauli kwa pikipiki ni Tshs. 1,000/= tu hadi shulenii. Kwa wanafunzi wanaotoka kata ya kilangawana na kipeta, usafiri ni pikipiki na nauli yake ni maelewano ya abiria na dereva kulingana na sehemu anapotokea mwanafunzi. Kwa atakayeshindwa kuelewa kwa sababu ya ugeni naomba tuwasiliane kwa namba ya simu ya mkuu wa shule 0756275058/0718406870 au makamu mkuu wa shule 0768060850.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 11.01.2021. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule tarehe 11.01.2021

Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wazazi wote ambaohawatawaleta watoto wao shule ifikapo tarehe 14.01.2021.

1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

1.0 Sare za shule

- 1 Sare ya shule hii ni suruali mbili (damu ya mzee na dark-blue) kwa wavulana na skirt mbili (damu ya mzee na dark-blue) kwa wasichana, mashati mawili meupe mikono mifupi kwa wavulana na wasichana. Sare ya michezo kwa shule hii ni bukta 2 rangi ya blue na tracksuit pair moja kwa wavulana na wasichana ni tracksuit pair moja.
2. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
3. Soksi jozi mbili wavulana Nyeusi na wasichana nyeupe.
4. Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi kwa wavulana tu.
5. Sweta pair 2 (damu ya mzee 1 na blue 1)
6. Nguo za kushindia (shamba *Dress*) suruali 1 kijani kibichi (wavulana), skirt 1 kijani kibichi (wasichana) na T-shirt ya kola (form six) ya blue yenye kola nyeupe na ufito mweupe mwishoni mwa mikono au sweta 1 ya blue la round kola.
7. Tai 2 (dark blue 1 na damu ya mzee 1)

1.1 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shulen ni:-

- 1 Meza 1 na kiti 1 (**vya chuma**)
- 2 Godoro 1 foot mbili na nusu kwa watakaolala hostel.
- 4 Mashuka pair 2 (rangi ya pink), blanketi 1 kwa wanaohitaji, foronya 1 (rangi ya pink) na chandarua 1.
- 5 Daftari kubwa 12 (quire 2 au 3).
- 6 Mathematical set 1.
- 7 Pencil 2 na pen za kutosha.
- 8 Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na Kikombe) wa hostel tu.
- 9 Ndoo mbili ndogo zenyne mifuniko
- 10 Kwanja 1, jembe1, reki1, mfagio 1 wa ndani na mfagio 1 wa nje.
- 11 REAM 1.

2 GHARAMA ZA CHAKULA KWA WATAKAAOKAA HOSTEL.

1. Mahindi gunia 2 kwa mwaka (unaweza kuleta debe tatu tatu kila robo muhula)
2. Maharage debe 4 kwa mwaka (unaweza kuleta debe moja moja kila robo muhula)
3. Mchele debe 2 kwa mwaka (unaletwa kipindi cha mavuno)
4. Fedha TSHS. 80,000/= kwa mwaka (unaweza kulipa TSHS. 20,000/= kila muhula).

3 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule ya Sekondari Kipeta inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenyeye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli utakazopewa ndani na nje ya shule.
- Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni (Preparation).
- Kuwahi katika shughuli za shule na nyininge utakazopewa.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- Kuvalaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

3. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

- (i) Wizi
- (ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro
- (iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
- (iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
- (v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu ye yote Yule.
- (vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika, Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
- (vii) Kufuga ndevu
- (viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
- (ix) Uvutaji wa sigara.
- (x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
- (xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
- (xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- (xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
- (xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
- (xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- (xvi) Kudharau Bendera ya Taifa.
- (xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- (xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo hayo na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KIPETA SEKONDARI.

Saini ya Mkuu wa Shule _____
Jina la Mkuu wa Shule: DELIGO LUPOLA

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIPETA
SL.P.78 SUMBAWANGA

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND
VOCATIONAL TRAINING

KIPETA HIGH SCHOOL,
P.O. BOX 78,
SUMBAWANGA.

DATE.....

MEDICAL OFFICER

.....
.....
.....
.....

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR.....
(NAME OF STUDENT)

Please examine the above named as to his/her fitness as indicated below. Arrange the necessary treatment so that the certificate may be brought to school by the student.

This certificate must be signed by a qualified Medical Officer of a recognized Government hospital.

1. Hemoglobin
2. (a) Bleeding
- (b) Hearing
3. Blood pressure
4. Stool for routine examination
5. Skin diseases
6. Pulmonary tuberculosis
7. Peptic ulcers.....
8. Eyes problem
9. Mental problem
10. Comment.....

.....
Name of medical officer..... Signature..... Date.....

Official stamp